Mama yake alimpiga

Tazama: Naja—
upesi
Ufunuo 22:12

Galina alizaliwa katika kijiji kimoja katika Asia ya Kati lakini alikuwa na ugonjwa wa uti wa mgongo. Galina ana kaka na dada wanane na kutokana na ulemavu wake huo alipata elimu ndogo sana.

Alifichwa jirani wasimwone

Hadi alipofikia umri wa miaka kumi, alikuwa akikaa nyumbani. Wazazi wake walimwonea aibu na hawakuruhusu marafiki wala majirani kumwona. Mama yake alimpiga mara kwa mara kwa vile hakuweza kudhibiti mambo yaliyokuwa yakifanywa na mwili wake. Hii ilimfanya afikiri kwamba huo ulemavu ulikuwa ni kosa lake. Hivyo alijisikia vibaya sana. Alidhani kwamba kulikuwa na dhambi ambayo alikuwa ameifanya.

svc.hu

Miaka minne iliyofuata alikaa hospitali. Alipokuwa na umri wa miaka 14, alipelekwa katika nyumba ya walemavu. Alipapenda zaidi pale kwa vile alikutana na wenzake waliokuwa walemavu kama yeye. Hakujiona ni mtu wa tofauti na wenzake.

Lakini kila aliporudi nyumbani kwao, aligundua jinsi alivyokuwa tofauti na kaka na dada zake. Alikosa furaha kiasi kwamba alijaribu kujiua lakini hakufanikiwa. Mara baada ya hili, alitoroka nyumbani na kukimbilia mjini. Huko alipata kazi katika kiwanda.

Marafiki wapya

Galina alipokuwa akifanya kazi mjini, kundi la Wakristo lilimtembelea. Walimweleza habari za Yesu Kristo anayewapenda watu wote hata wale wenye ulemavu. Hakuyapenda mambo ya dini kwa vile alipokuwa mdogo alielezwa na kufundishwa habari za dini nyingine.

Lakini Wakristo hawa hawakukata tamaa kumtembelea. Galina aliendelea kuwa rafiki yao japokuwa hakupenda mambo waliyokuwa wakiyasema. Kwa miaka nane, aliona jinsi hawa Wakristo walivyoishi na jinsi walivyomjali. Walimpenda hivyohivyo alivyokuwa.

Kisha alianza kutambua kwamba rafiki yao Yesu Kristo, alimpenda kiasi kwamba alikufa kuchukua adhabu ya dhambi zake. Lilikuwa ni pendo la Yesu ambalo wale rafiki zake walimwonyesha kwa miaka yote hiyo. Alimwomba Yesu ayabadilishe maisha yake na kumjaza upendo, furaha na amani. Alimpata rafiki mpya ambaye ni Yesu.

Galina hajisikii kukataliwa tena. Sasa haogopi tena maisha ya baadaye. Anajisikia kukubalika na kupendwa na Mungu. Uhusiano wake na wazazi wake pia umebadilika. Wameona jinsi ambavyo maisha yake yamebadilika na kuwa bora zaidi.

Upendo mpya

Wakati fulani alipoenda kuwaona wazazi wake, mama yake alimwomba Galina amsamehe kwa jinsi alivyompiga mara nyingi alipokuwa mtoto. Sasa wazazi wake wanampenda, jambo ambalo hakuwahi kuliona katika maisha yake.

Yesu amebadilisha kabisa maisha ya Galina. Sasa ni mwanamke mwenye furaha na anawasaidia wanawake wengine walemavu ambao ni maskini sana na wasio na mikongojo au viti vya baiskeli.

Watu wengi, kama Galina alipokuwa mdogo, hawawezi kutoka katika nyumba zao. Anaelewa jinsi walemavu wanavyojisikia na matatizo wanayoyapata. Mungu amempa huduma maalum ya kufanya.

Jambo la kufikiri

Inawezekana wewe si mlemavu kama Galina, lakini watu wengi ni 'walemu' kwa njia nyingine nyingi. Inawezekana ulijeruhiwa au kutumikishwa ulipokuwa mtoto. Inawezekana hukupata elimu ambayo uliitegemea. Inawezekana huwezi kufanya mambo unayopenda kwa sababu familia yenu ni maskini au kwa sababu wazazi au mzazi alifariki ulipokuwa mdogo. Kuna sababu nyingi zinazokufanya ujifikirie vibaya. Je, ni jambo gani Galina aliloona lililoleta hayo mabadiliko yote katika maisha yake?

Ugonjwa wa uti wa mgongo

Ugonjwa wa uti wa mgongo uitwao Spina Bifida ni ugonjwa unaompata mtoto akiwa angali tumboni mwa mama yake. Mifupa ya uti wa mgongo inakua vibaya. Kwa hiyo, haiulindi uti wa mgongo na mfumo wa fahamu wa mwili mzima ulio sawa. Mtoto anayezaliwa na hali hii huenda asiweze kusikia baadhi ya hisia za mwili wake au akashindwa kufanya mambo fulani. Kwa mfano, hawezi kutembea sawasawa au kufanya mambo vizuri kama mtu mwingine.

Kutoka kwa wasomaji

Peter Yohana kutoka Tanzania:

Ninapenda kutoa shukrani nyingi sana kwa jarida la *UPESI*. Limenibariki na kunibadilisha na kunisaidia katika kumjua Mungu zaidi.

Kupitia *UPESI*, nimeona maajabu na shuhuda nyingi sana na ishara kubwa ambazo Mungu amefanya kwa watu katika mataifa mbalimbali.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunijenga kiroho kupitia jarida la *UPESI*. Nimekuwa nikiwagawia jarida hilo watu wengine ambao hawajampokea Yesu. Wanafurahia sana kusoma *UPESI*, na ninajua kuwa ninapanda mbegu njema, na mavuno yako karibu.

Ombi langu ni kuwa, ninahitaji majarida ya *UPESI* mengi zaidi ili niendelee kuyagawa kwa watu ambao hawajamwamini Kristo. Kama kuna vijitabu au kalenda kuhusu mafundisho ya Biblia, naomba mnitumie ili niweze kujiendeleza katika kumjua Mungu zaidi.

Veronicah Nyaguthii kutoka Kenya:

Mimi ni msichana wa miaka 17. Mimi niliona kuwa hakuna haja ya wokovu kwa msichana kama mimi. Niliona kwamba urembo wa usichana wangu ulikuwa na thamani kuliko wokovu wa Mungu. Hata hivyo, Mungu ni mwema na mwenye huruma kwa maana alinifunulia kuwa urembo wa usichana utapita, bali Neno lake litasimama hata milele. Isaya 40:6-8 inasema, **"Sikiliza, ni sauti ya mtu asemaye, Lia! Nikasema, 'Nilie nini?' Wote wenye mwili ni majani, na wema wake wote ni kama ua la kondeni; majani yakauka, ua lanyauka; kwa sababu pumzi ya BWANA yapita juu yake. Yakini watu hawa ni majani. Majani yakauka, ua lanyauka; bali Neno la Mungu wetu litasimama milele."**

Roho yangu ilivunjikavunjika sikuona haja tena ya urembo wangu. Kwa hiyo, nilimkimbilia Bwana Yesu. Naye kwa kuwa ni mwingi wa huruma, akanipokea na kuniokoa. Namshukuru kwa wokovu wake na ufunuo wake wa wokovu ambao amenipa. Nitamwishia Mungu aliyeniokoa. Amina.

Kata hapa

Jina..... Umri: .....

Anwani.....

.....

Nchi.....

Andika e-mail yako hapa, ukiwa nayo: .....

116

- UKITAKA KUPOKEA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, jaza na ututumie cheti hiki nasi tutakutumia bure nakala ya *UPESI* kwa mwaka.
- **Andika jina na anwani yako kwa HERUFI KUBWA. Kisha tuma kwa: *UPESI*, Willington, Derby, England, DE65 6BN**
- Ukituma barua bila stampu, au ukitumia stampu zisizo mpya, barua haitatufikia.
- Ukitaka kusoma *UPESI* kwenye INTERNET, tumia: http://soon.org.uk/swahili/swahili.htm
- Ili kupokea magazeti ya *UPESI* kwa njia ya posta tafadhali andika na kutuma anwani yako kwa: upesi-office@soon.org.uk
- Ili kupokea gazeti la *UPESI* kwa njia ya email, tafadhali tuma email isiyoandikwa chochote kwa hii awani, upesi-subscribe@soon.org

ISSN 1472-7285

Mhubiri ndani ya basi

Ilikuwa Ijumaa ya tarehe 23 Juni 2007. Nilikuwa nikisafiri kutoka katika wilaya ya Kpambo ambayo ni wilaya ya nyumbani kwenda wilaya ya Kwabu ambayo iko katika jimbo la Taraba nchini Nigeria.

Huwa napenda kusafiri kwa kutumia basi. Kwa hiyo nilienda kituo cha basi na kusubiri pale kama dakika sita hivi. Basi lenye watu 40 lilikuja na kunichukua pale. Ndani ya basi kulikuwa na mtumishi wa Mungu ambaye ni Mwinjilisti Rmam Skapki ambaye alikuwa akifanya kazi ya kuhubiri kwenye mabasi.

Safari yetu ilianza na tulipokuwa tumesafiri maili moja kutoka Kpambo, mtumishi huyo wa Mungu alisimama toka alikokuwa amekaa. Kisha alisema, *"Nawasalimuni nyote katika jina la Yesu ambaye ni Bwana na Mwokozi wetu."* Pia akasema, *"Na tuiweke safari yetu hii mikononi mwa Mungu."* Alifanya sala fupi kisha akaanza kuimba nyimbo za kusifu na kuabudu. Wenye hali ya bidii wakajiunga naye.

Aliyachukia mahubiri ya Kikristo

Baada ya muda alituelekeza kwamba tuache kuimba na akaanza mahubiri kutoka katika Neno la Mungu, kitabu cha Matendo sura ya 9. Alipokuwa akisoma, mtu mmoja mwanaume aliyekuwa ameketi katika kiti cha upande wa mbele, akaanguka na kuanza kulia huku akitubu makosa aliyokuwa akitenda dhidi ya waamini. Hakuna aliyeweza kujua ni nini kilichokuwa kinamtokea.

Tulikuja kugundua baadaye kuwa huyu mtu alikuwa ni mganga maarufu wa kienyeji katika eneo lote la Kwabu. Kwa kweli mganga huyo aliwachukia Wakristo na mahubiri yao na hakupenda hata Mkristo amsogelee.

Kwa bahati mbaya sana siku hiyo huyu mtumishi wa Mungu alisafiri naye gari moja na alikuwa anataka kuanza kuhubiri. Na kweli huyo mganga hakutaka kuona hili likitokea mahali alipo. Kwa hiyo alivyoeleza, alitaka kuleta mapepo ili yasababishe ajali. Mara Roho wa Mungu aliingilia kwa sababu Mungu alisema mipango mibaya itakayopangwa dhidi yake haitafanikiwa.

Hata hivyo, huyo mganga alitubu makosa aliyokuwa ameyafanya hapo awali mbele ya umati ule na kuomba msamaha mara moja. Kwa hiyo, ili asiyarudie tena matendo yake ya awali aliondoka katika wilaya ya Kwabu ambako ni nyumbani na kwenda mji mwingine ambako sasa ni mwamini mzuri sana wa Kikristo.

Sikiliza Redio!

Sikiliza Habari Njema katika lugha ya Kiswahili:

Redio Habari Maalum: 11885 kHz, Metabendi 25, kila siku

TWR: 9475Khz MB 31, 1700-1800 UTC
6110Khz MB49, 0300-0330 UTC

IBRA: 9520Khz MB31, 1730-1830 UTC

Mombasa-Baraka FM – Kwenye 95.5FM katika Kiswahili na Kiingereza
Na kwenye vipindi vya **FM** nyingi
Ukipenda kuona nyingine, tazama:
www.soon.org.uk/radio

Mlo wa wizi

Mfano mfupi toka kwaThomas, Nigeria

Miaka mingi iliyopita kulikuwa na shule ambayo wanafunzi wake walikuwa na tabia mbaya sana kiasi kwamba hakuna mwalimu aliyeweza kuwafanya wawe wasikivu. Wavulani walikuwa wakorofi hadi walimu wakawa wanaondoka mmoja baada ya mwingine.

Mwalimu mpya

Kisha siku moja, kijana mmoja alikuja kufanya kazi hiyo. Mwalimu mkuu alimtazama. Akasema, *"Kijana, unajua kitakachotokea kwako? Utapigwa mara nyingi na wanafunzi. Kwa miaka mingi, kila mwalimu shuleni hapa aliteseka kwa jinsi hiyo."*

Yule kijana akajibu, *"Niko tayari kujitia kwenye hatari hiyo."*

sepal.org/gulick

Mwalimu huyo mpya alipoanza kazi, Samweli, mmoja wa wavulana wakubwa, alinong'ona, *"Sitahitaji msaada wowote. Naweza kumpiga mimi mwenyewe."*

Mwalimu alisimama mbele ya darasa na kusema, *"Hamjambo? Nimekuja kuwafundisha, lakini nitahitaji msaada wenu. Hatuwezi kuwa na shule bila kutengeneza japo sheria chache. Mniambie sheria ziwe ni nini nami nitaziandika ili wote mzione."*

Sheria za shule

Mwanafunzi mmoja alisema, *"Hakuna kuiba."* Mwingine akasema, *"Usichelewe darasani."* Hatimaye wakawa na sheria kumi.

"Sasa," alisema mwalimu, *"sheria haina maana hadi tukubaliane kuhusu adhabu. Je, mtu atakayevunja sheria afanywe nini?"*

"Mpige mgongoni mara kumi akiwa amevua koti," alipaza sauti mvulana mmoja.

"Hiyo ni adhabu ngumu sana, kijana. Mtaniruhusu kufanya hivyo kama mtu akivunja sheria?"

"Ndiyo," walijibu darasa zima.

Sheria ikavunjwa

Siku chache baadaye, chakula cha mchana cha Samweli kiliibwa. Mwizi akaonekana kuwa ni Yakobo, mvulana mdogo wa miaka kumi mwenye njaa. Asubuhi iliyofuata mwalimu alisema darasani, *"Tumempata mwizi na ni lazima aadhibiwe. Sheria yenu inasema kwamba ni lazima apigwe viboko kumi mgongoni. Yakobo, njoo hapa!"*

Huku akitetemeka, Yakobo alikuja taratibu mbele ya darasa. Alivaa koti kubwa lililofungwa vifungo hadi shingoni. Alisema, *"Mwalimu, unaweza kunipiga kwa nguvu upendavyo, lakini tafadhali usinivue koti langu."*

"Vua koti. Ulisaidia kutunga sheria!"

"Ee, mwalimu, usinivue!" Alianza kufungua vifungo vya koti lake. Je, mwalimu na darasa zima waliona nini? Mvulana huyo hakuwa na shati isipokuwa kamba tu ya kushikilia suruali yake. Mwili wake ulikuwa mwembamba na mkondefu.

"Nitampigaje mvulana huyu?" aliwaza mwalimu. *"Lakini lazima nifanye jambo kama nataka amani iwepo shuleni."* Kila kitu kilikuwa kimya darasani.

"Kwa nini umekuja shuleni bila shati, Yakobo?" aliuliza mwalimu.

Yakobo akamjibu *"Baba yangu alishakufa na mama yangu ni maskini sana. Nina shati moja tu na mama yangu analifua leo. Nimevaa koti la kaka yangu ili nipate joto."*

Mbadala

Mwalimu, huku akiwa na fimbo yake mkononi, alisita. Mara, Samweli alisimama na kusema, *"Mwalimu, kama ukikubali, mimi nitapigwa badala ya Yakobo."*

"Ndiyo, kuna sheria inayosema kuwa mtu anaweza kubeba adhabu ya mwingine, anaweza kuwa mbadala. Je, wote mnakubaliana?" aliuliza mwalimu.

"Ndiyo," walijibu darasa zima.

Samweli alivua koti lake. Baada ya viboko vitano vya nguvu, fimbo ilivunjika. Mwalimu alificha kichwa chake kwenye mikono yake na kuwaza, *"Nawezaje kuimaliza kazi hii ya kutisha hivi?"*

Mara akasikia shule nzima ikilia. Mvulana mdogo Yakobo aliinuka na kumkumbatia Samweli shingoni. *"Samweli, unisamehe kwa kukuibia chakula chako, lakini nilikuwa na njaa sana. Samweli, nitakupenda hadi siku ya kufa kwangu kwa sababu umebeba adhabu yangu. Nitakupenda daima."*

Hiki ndicho ambacho Yesu alifanya kwa ajili yetu.

Nilikuwa na mzigo mzito

Jina langu ni Nemoomsa Yadeta. Mimi ni Muethiopia. Nilikuwa mwalimu kwa miaka zaidi ya ishirini, lakini sasa nafanya kazi katika ofisi.

Nilikutana na mke wangu pale tulipoanza wote kufundisha kwenye shule moja. Tulipooana tu tulipendana sana. Tulipata watoto watatu, lakini kadiri muda ulivyoendelea, ndoa yetu haikuwa inaenda vizuri. Baada ya miaka tisa, mke wangu aliniacha. Ndoa yetu iliishia kwenye talaka.

sxc.hu

Niliachwa na wale watoto watatu. Haikuwa rahisi kwangu kuwalea watoto watatu, lakini Mungu alinisaidia.

Nilioa tena

Miaka sita baada ya kutalikiana na mke wangu wa kwanza, nilioa tena. Mke wangu huyu alikuwa mzuri sana kwa kila hali, lakini kwa masikitiko, alikufa. Hii ilifanya maisha yangu yawe magumu sana kuyabeba. Nilihisi kama vile nimebeba mzigo mzito sana mgongoni mwangu. Wakati wa miaka hii migumu, nilimshukuru Mungu kila siku, hata pale mambo yalipokuwa hayaniendei vizuri. Wakati mmoja Mungu alinisaidia kujenga nyumba yangu tena pale ilipobomoka. Nilijua Mungu alikuwa nami na alikuwa akinisaidia.

Usikate tamaa kamwe

Hivi sasa wanangu wote wamekua. Sina tena huo mzigo mzito, lakini nimejifunza kuwa hata kama tukikutana na matatizo mengi, tusipoteze tumaini kamwe. Tunapomwomba Mungu awe rafiki yetu na kumshukuru kila siku, atatusaidia katika matatizo na mizigo mizito tuliyo nayo maishani.

Jifunza kitabu cha Mungu

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina na anwani yako kwa:

Katika KENYA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 72725, Nairobi, Kenya

Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Rép. Dém. du Congo

Katika TANZANIA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 1424 Dodoma, Tanzania. Wanasubiri barua yako ili uweze kutumiwa somo lako la kwanza bila malipo.